MISINGI YA MAISHA

KANUNI 50 ZA MAISHA YA MAFANIKIO



Yatoe maisha yako kwa kitu fulani

DENIS J. MSANGI

Toleo la kwanza
Hakimiliki © 2023

Denis Jonas Msangi
Simu: +255715922392/+255627668898
Barua pepe: dennlyson@yahoo.com
Dar es Salaam
Tanzania.

Mhariri
Jabir Abdallah Mvamila
Simu: +255627668898
Barua pepe: jmvamila@yahoo.co.uk
Dar es Salaam

Sanifu jalada na ubunifu wa ndani ya kitabu
DL Bookstore
Simu: +255787163013
Baruapepe: authors@dlbookstore.com
Tovuti: www.dlbookstore.com
Arusha
Tanzania.

Jopo la wataalam wa The Institute of Professionalism and Montessor Education
Baruapepe: jonasdenis52@mail.com

ISBN 978 9987 93 326 6

Kitabu hiki cha Kanuni za Maisha ya Mafanikio ni mali ya Denis Jonas Msangi, siruhusa kunakili au kuiga kwa njia yoyote ile pasipo na ruhusa ya mmiliki. Hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mtu yoyote atakae kiuka ilani hii.

YALIYOMO

Shukrani.....vii
Utangulizi ix
Jifunze Kuyaweka Moyoni Yaliyo Yako 1
Kuwa Na Fikra Za Mabadiliko..... 3
Yatoe Maisha Yako Kwa Kitu Fulani..... 7
Kuwa Mshauri Wa Mambo Yako 9
Ukifikiri Unaweza Kufanya Hiki, Fikiri Uwezo Wa Kufanikisha.. 11
Fikiri Kuwa Wa Kwanza Bora Na Si Wa Pili Bora..... 13
Usiogope Kuwa Na Ndoto..... 15
Kua Mtu Wa Mipango..... 17
Kuwa Na Mwongozo Wa Kufanikiwa..... 19
Kuwa Na Mipango Katika Matarajio Yako Ya Kazi..... 25
Kuwa Na Mipaka Yako Ya Maisha..... 27
Kutumia Fedha Katika Matatizo, Si Wakati Wote Husaidia..... 31
Tafuta Fedha Kwa Vile Unavyovihitaji Sio Unavyotaka 33
Jaribu Kutunza Afya Yako 35
Kuwa Na Mwelekeo Katika Matarajio Yako..... 39

Jikubali Ulivyo 43
Kuwa Na Uwezo Wa Kujiongoza 45
Kuwa Mwema Kazini Kwako 49
Kuwa Mtu Wa Kusamehe 51
Yafanye Maisha Yako Yafaidike Na Ulimwengu Uliopo 53
Badilisha Yanayowezekana, Mengine Yaache Yapite 55
Usiumie Kwa Yaliyopita 57
Usiishi Kwa Wakati Ujao Na Wa Baadae 59
Jipatie Muda Na Nafasi Kwa Ajili Yako Tu Kila Siku..... 61
Jifunze Kuuliza Maswali 63
Fahamu Kuwa Huwezi Kufahamu Kila Kitu 65
Fahamu Lini Kuyaacha Yapite Na Lini Kuyakimbia Na Kutafuta Mwelekeo Mpya..... 67
Kama Unaanza Urafiki Jaribu Kuwa Rafiki Mwema..... 69
Kuwa Na Tabia Ya Kusaidia..... 71
Fahamu Kilicho Bora Na Yasiyo Bora 75
Ishi Katika Mazuri Na Sio Katika Mabaya..... 77
Fahamu Mahali Furaha Yako Ya Kweli Ilipo 79
Jiangalie Wewe Mwenyewe 81
Nunua Vilivyo Bora Na Sio Gharama 83
Jifikirie Wewe Mwenyewe..... 85
Kuwa Na Kitu Katika Maisha Kinachokupa Raha Ya Kuishi 87
Usihisi Kutengwa Na Wengine..... 89

Kuwa Mwenye Kukabiliana Na Misongo 95
Kawaida Kuwa Na Hisia Kali 101
Angalia Historia Itakuzungumziaje Baadaye 105
Kuwa Wa Mwisho Kutoa Sauti Yako 107
Yaliyotendeka, Yametendeka Kubaliana Nayo 109
Kuvaa Kwa Wakati Ni Muhimu Pia..... 111
Chagua Namna Ya Kupanga Kitanda Chako..... 113
Jifunze Kuwa Na Tabia Nzuri Kwa Kila Kitu..... 115
Baki Na Muonekano Wa Ujana 117
Kama Huwezi Kuongea Mazuri, Basi Usiongee Kabisa..... 119
Jifunze Kuona Jamii Yako Katika Mtazamo Mpana Zaidi 121
Yapo Matarajio Yasiyotimizwa Katika Maisha 123
Wewe Sio Mwezeshaji Wa Maisha Yako..... 127

SHUKRANI

Kwanza ninapenda kumshukuru Mungu muumba mbingu na ardhi kwa kunipa afya na busara ya kufikiri na akili ya kuandika kitabu hiki. Pia ninapenda kuishukuru familia ya Lilian Doris Mawani kwa malezi na ushauri hadi kufanikisha kitabu hiki kukamilika na ninaiombea maisha Bora na ya Mafanikio.

Pili napenda kumshukuru Jabir A. Mvamila kwa ushauri mkubwa na msaada mkubwa wa mawazo na kiufundi hadi kufikia hapa kitabu kilipofikia. Namtakia maisha marefu na mafanikio awe mvumilivu. MAISHA NI CHANGAMOTO NA MAPAMBANO. Pia napenda kuishukuru ofisi ya Montessori Teachers taining college na wafanyakazi wake wote kwa ushirikiano wao kimawazo pamoja na changamoto zao katika kukamilisha kanuni za maisha.

Sitakua kua mwingi wa fadhila nikimsahau Anna Jonas Mremi kwa ushauri, ushirikiano, hamasa na kunipa moyo hadi kufikia hapa, akumbuke kua Maisha ni uvumilivu, upendo na mshikamano pasipo kukata tamaa.

Na shukrani za dhati ziwaendee wale wote wa karibu waliochangia kwa namna moja au nyingine katika kukamilisha kitabu hiki pamoja na wanunuaji na wasambazaji wa kitabu hiki. Ninawatakia maisha mema na ya mafanikio

UTANGULIZI

Kitabu cha KANUNI ZA MAISHA YA MAFANIKIO ni kitabu kilicholenga kuwaongoza watu kutambua maisha yao na jinsi wanavyoweza kufurahia maisha yao ya binafsi, familia ,jamii na ya mahusiano, kujua ambavyo wewe pamoja na wanaokuzunguka kufurahia kwa pamoja na kuepukana na misongo ya mawazo.

Anza leo kuwa mmoja wa wasomaji wa kitabu cha KANUNI ZA MAISHA YA MAFANIKIO ili kufanya maisha yako yawe ya furaha, amani, na upendo. Kitabu hiki kimejaribu kuweka kanuni mbalimbali zitakazosaidia kujua namna mtu anavyoweza kuishi na kukubaliana na ya ulimwengu.

Kumbuka ulimwengu ni kama nguo, siku ya kuinunua huonekana vyema na kadri siku zinavyokwenda ndivyo hupunguza mapenzi nayo. Kanuni za maisha hukusaidia kila siku ujaribu kuyaona maisha katika utofauti wa nguo uliyoinunua na kuendelea kufurahia maisha zaidi kila siku.

Ni wazi kuwa maisha ni majumuisho wa mambo mengi mazuri na mabaya ndani yake ambayo binadamu kila siku hukumbana nayo, yapo mazuri kama kuoa, kuolewa, kupata mali, watoto na marafiki uliowazoea na kuwapenda,

Yapo mabaya ambayo tunakumbana nayo kutwa kuchwa kama, vifo, ugonjwa, umaskini, njaa na hata kuudhiwa na marafiki na ndugu tulio nao. Kitabu hiki kimejaribu kuonyesha vile ambavyo tunaweza kukabiliana na yote haya na kupata nafasi ya kuishi kwa furaha, afya na upendo. Kuwa sasa miongoni mwa wasomaji wa kitabu hiki ili uweza kuyafanya maisha yako yawe ya utajiri, afya, furaha, amani ya moyo na upendo kwako binafsi na wanao kuzunguka kufurahia uwepo wako duniani.

KARIBU KUWA MMOJA WA KANUNI ZA MAISHA YA MAFANIKIO

1

JIFUNZE KUYAWEKA MOYONI YALIYO YAKO

Ukikubali kufuata mipango yako ya maisha utakuwa ni miongoni mwa watu waliogundua njia za kuwa watu chanya, wenye furaha na mafanikio kwa kila wanachokifanya. Cha msingi ni kutokuwa muwazi kwa kila unachofanya au kutaka kukifanya kwa wengine, kuwa mtulivu na kinywa chako kwa yale muhimu unayotaka kuyafanya. Kwa kawaida watu wengi hawapendi kusikia mipango yako mizuri ya maisha

Weka moyoni mambo yako na wafanye watu watafute wenyewe kile unachokifanya, hakuna ulazima wa wewe kushirikisha watu kwa kila kitu, wengi hupenda kuuliza nini wenzao wanafanya na si rahisi wao kusema nini wao wanafanya, hakuna ulazima wa wewe kujieleza, hivyo ni bora useme 'HAKUNA' kwa sababu watu hawapendi maelezo kuhusu mambo yako.

JIFUNZE KUYAWEKA MOYONI YALIYOYAKO
KWAKUA WENGI HAWAPENDI KUSIKIA MIPANGO
YAKO MIZURI